

**ABIRIA WOTE KUVAA BARAKOA WAKATI WOTE WA SAFARI
KATIKA KIPINDI HIKI CHA COVID-19
21 APRILI, 2020**

Uongozi wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) unapenda kuwataarifu wateja wake na umma kwa ujumla kuwa kuanzia sasa abiria wote watakao safiri au kutumia huduma zetu wanatakiwa kuvaa barakoa kabla na wakati wote wa safari. Aidha abiria na wateja wetu wote hawatahudumiwa katika vituo na ofisi zetu mahali popote bila kuwa wamevaa barakoa.

ATCL tunaendelea kuchukua tahadhari zote za Kiusalama, ili kuhakikisha afya za wafanyakazi, abiria na wateja wetu wote kwa ujumla, zinalindwa kama inavyoelekezwa na Wizara ya Afya.

ATCL tunaendelea kutoa huduma katika safari za ndani katika vituo vyote 11 ambavyo ni Dar es Salaam, Zanzibar, Kilimanjaro, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Tabora, Dodoma, Mpanda, Iringa na Mbeya pia tumeanzisha safari ya kwenda na kurudi baina ya Kilimanjaro na Mwanza.

Tunawakumbusha wateja wetu kufanya maandalizi ya safari zao kupitia mtandao wetu wa www.airtanzania.co.tz na kufanya malipo kwa Tigopesa, Mpesa, kadi za Benki au kwa wakala wako ili kupunguza muda na kuepuka misongamano isiyo ya lazima.

Tunawaomba radhi wateja wetu kwa usumbufu unaojitokeza katika kipindi hiki cha COVID-19. Kwa taarifa na ufafanuzi zaidi usisite kuwasiliana nasi kupitia **0800110045**.

Safiri Salama, Fika Salama



Mhandisi Ladislaus Matindi
MKURUGENZI MTENDAJI